

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**



**TAARIFA KWA UMMA**

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anawatangazia wamiliki wote wa ardhi nchini kuwa, kwa mujibu wa Fungu la 33(1) la Sheria ya Ardhi, wanatakiwa kulipa kodi ya pango la ardhi kila mwaka. Kodi hiyo inapaswa kulipwa katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Halmashauri zote nchini. Muda wa kulipa kodi ya pango la ardhi bila riba unaanzia tarehe **moja mwezi wa saba mpaka tarehe thelathini na moja mwezi wa kumi na mbili kila mwaka**. Baada ya tarehe hiyo, kodi ya pango la ardhi italipwa pamoja na riba.

Kwa sababu hiyo, wamiliki wote wa ardhi nchini mnatakiwa kulipa kodi ya pango la ardhi na malimbikizo yote ifikapo tarehe **31.03.2015**. Ikumbukwe kuwa, kutolipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati ni ukiukwaji wa masharti ya umiliki wa ardhi ambao madhara yake ni pamoja na kunadiwa mali au kufutiwa umiliki wa ardhi.

Kwa muda mrefu Wizara imekuwa ikiwakumbusha wamiliki wa viwanja/mashamba nchini kulipa kodi ya ardhi kwa wakati bila mafanikio. Umiliki wa ardhi unaendana na wamiliki kukidhi masharti ya uendelezaji na umilki wa ardhi. Hivyo basi, baada ya muda uliotangazwa hapo juu kupita, Wizara itawatangaza kwenye vyombo vya habari wamiliki wote ambao watakuwa hawajalipa kodi ya pango la ardhi bila kujali wasifu wao sanjari na kuwachukulia hatua stahiki za kisheria. Hakutakuwa na kumbusho lingine tena juu ya suala hili.

Imetolewa na:

Mhe. William V. Lukuvi (Mb.)  
**WAZIRI WA WIZARA YA ARDHI, NYUMBA  
NA MAENDELEO YA MAKAZI**